# BRIGHT STAR PRE AND PRIMARY SCHOOL

**P.O BOX 360 MAKAMBAKO, NJOMBE**

*CELL. 0766617497/0714702045*

*Email. brightstarschooltanzania@gmail.com*

*Website. www.brightstarsschools.co.tz*


---

## FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE KWA MWAKA WA MASOMO 2026.

### UTANGULIZI.

Bright star Pre & Primary School ni shule ya elimu ya msingi na awali yenye usajili **EM 18307**. Inapokea watoto kuanzia elimu ya msingi na awali mwaka wa masomo 2026. Shule inapatikanakatika mtaa wa Mashujaa - kata ya Kivavi, Makambako mjini.

**Huduma zitolewazo;**

- ✓ *Elimu ya msingi na awali.*
- ✓ *Chakula kwa mtoto (Milo mitatu mwanafunzi akiwepo shuleni: Asubuhi, mchana nakabla ya kurudi nyumbani ) .*
- ✓ *Tuna michezo mbalimbali kwa ajili ya kuchochea ubunifu na ushirikiano.*
- ✓ *Shule hii ipo katika mazingira mazuri yenye utulivu kwa malezi bora ya mwanao (Mazingira ni safi, maji ya kutosha, sakafu na kuta safi zitakazomuweka mwanao katika hali ya usafi wakati wote awapo shuleni).*
- ✓ *Pia tunatoa huduma ya usafiri kwa mwanafunzi kwa kuchukuliwa katika vituo au kufuatwa na kurudishwa hadi nyumbani.*
- ✓ *Shule ina uzio pamoja ulinzi wa kutosha.*
- ✓ *Shule ina walimu bora katika utoaji wa elimu na malezi.*

Tunaamini watoto wetu ni hazina kubwa tuliyopewa na Mungu tunahitaji ushirikiano wa karibu kwa wazazi na walimu ili kuleta mafanikio makubwa katika malezi, taaluma na maadili kwa mtoto. ***KARIBU SANA.***

### UTARATIBU WA KUJIUNGA

Ili Kujiunga na shule hii, fomu za kujiunga zinapatikana shuleni Bright Star Pre & Primary School pia Bright Star Day care centre & Nursery school**.** Fomu ya maombi ni lazima iwe imejazwa kwa usahihi na mzazi/mlezi na kurudishwa shuleni kwa muda sahihi. Usajili wa mtoto utafanywa shuleni na si mahali pengine. Lugha ya kufundishia na mawasiliano ni kingereza (English).

## UTARATIBU WA MALIPO

Ada kwa darasa la 1, 2 na 3 kwa mwaka ni **Tsh 1,600,000/=** (masomo, chakula, na usafiri)

| AWAMU ZA MALIPO | MUDA WA MALIPO | KIASI CHA ADA (Tsh.) | JUMLA (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| MOJA | Januari | **1,600,000/=** | **1,600,000/=** |
| | | | |
| MBILI | Januari. | **1,000,000/=** | **1,600,000/=** |
| | Julai. | **600,000/=** | |
| | | | |
| TATU | Januari | **700,000/=** | **1,600,000/=** |
| | Aprili | **500,000/=** | |
| | Julai | **400,000/=** | |
| | | | |
| NNE | Januari | **550,000/=** | **1,600,000/=** |
| | Aprili | **500,000/=** | |
| | Julai | **400,000/=** | |
| | Septemba | **150,000/=** | |

Darasa la tano na la sita ada yao ni **1,750,000/-**

| AWAMU ZA MALIPO | MUDA WA MALIPO | KIASI CHAADA (Tsh.) | JUMLA (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| MOJA | Januari | **1,750,000/=** | **1,750,000/=** |
| | | | |
| MBILI | Januari. | **1,050,000/=** | **1,750,000/=** |
| | Julai. | **700,000/=** | |
| | | | |
| TATU | Januari | **750,000/=** | **1,750,000/=** |
| | Aprili | **500,000/=** | |
| | Julai | **500,000/=** | |
| | | | |
| NNE | Januari | **650,000/=** | **1,750,000/=** |
| | Aprili | **500,000/=** | |
| | Julai | **450,000/=** | |
| | Septemba | **150,000/=** | |

PRIMARY SCHOOL

| WANAFUNZI WA DARASA LA NNE NA SABA ada yao ni **2,150,000/=** | | | |
|---|---|---|---|
| **AWAMU ZA MALIPO** | **MUDA WA MALIPO** | **KIASI CHA ADA (Tsh.)** | **JUMLA (Tsh.)** |
| MOJA | Januari | **2,150,000/=** | **2,150,000/=** |
| | | | |
| MBILI | Januari. | **1,400,000/=** | **2,150,000/=** |
| | Julai. | **750,000/=** | |
| | | | |
| TATU | Januari | **855,000/=** | **2,150,000/=** |
| | Aprili | **745,000/=** | |
| | Julai | **550,000/=** | |

Mchanganuo wa 2,150,000 ni

| **DARASA** | **ADA** | **REMIDIAL** | **EXAMS** | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|
| CLASS IV | 1,850,000 | 150,000 | 150,000 | 2,150,000 |
| CLASS VII | 1,850,000 | 150,000 | 150,000 | 2,150,000 |

**N.B:** Ada hii inalipwa mapema kabla mtoto hajaanza masomo. Tafadhari malipo yote ya ADA yafanyike kwenye control number ya mtoto au Benki ya **NBC** Akaunti namba **055174000541 na CRDB** Akaunti namba **015C713349200** jina la akaunti zote ni **Bright Star Pre & Primary School**. Baada ya malipo utapaswa kuleta stakabadhi (risiti) ya malipo shuleni (**Original Bank Paying Slip**). Ada ikishalipwa haitorudishwa.

**TAMKO LA MALIPO**

Mimi_______________________________________mzazi wa _________________________ ninakubali na kuahidi kulipa ada kwa kufuata utaratibu uliowekwa na shule.

Saini ya mzazi_____________________Tarehe ___________________

## GHARAMA YA MAHITAJI MENGINE MUHIMU

Gharama kwa ajili ya mahitaji mengine ni kama ifuatavyo:

| ***KIFAA*** | | ***GHARAMA*** |
|---|---|---|
| Vifaa vya darasani kwa mwaka mzima | ***95,000*** | **355,000/=** |
| T-shirt 1 | ***85,000*** | |
| Sweta 1 | | |
| Track suit 1 | | |
| Socks pair 2 & Tie 2. | | |
| Usajili na tahadhari | ***70,000*** | |
| Diary/kitabu cha matokeo | ***5,000*** | |
| VITABU | ***100,000/=*** | |

- Mwanafunzi wa darasa la 1,2,3,5 na 6 atatakiwa kuleta ***limu Mbili*** aina ya **A4.**
- Darasa la ***NNE*** na la ***SABA*** wanaleta limu 3 aina ya ***A4***
- Malipo hayo ya shilingi **355,000/-** yafanyike katika akaunti ifuatayo.
  **055163007397** jina la akaunti ni **Bahati Abdallah Kiwambe**

## RATIBA YA SHULE YA MWAKA WA MASOMO 2026.

Mwaka wa masomo umegawanyika katika mihula miwili;

| **MIHULA** | **KUFUNGUA** | **KUFUNGA** |
|---|---|---|
| **KWANZA** | 13/01/2026 | 27/03/2026 |
| | 08/04/2026 | 05/06/2026 |
| | | |
| **PILI** | 06/07/2026 | 04/09/2026 |
| | 14/09/2026 | 04/12/2026 |

**Kwa mwaka wa masomo wa 2026 shule itafungua rasmi tarehe 13/01/2026**

**RATIBA YA SHULE KILA SIKU**

- Muda wa kuanza kuingia shuleni ni saa 1:00 asubuhi na mwisho wa kuingia shule ni saa 2:00 asubuhi baada ya hapo mtoto hatapokelewa. Kama kuna dharura yoyote itayomfanya mwanao kushindwa kufika shuleni tafadhari toa taarifa mapema shuleni kupitia simu namba **0714702045.**
- Kwa ushauri,maoni au malalamiko fika shuleni siku za kazi kuanzia saa 1:00 asubuhi – 6:30 mchana. Ikiwa shida hiyo ni ya dharura sana waweza kupiga simu ya shule namba **0714702045**. Simu hii ni ya ofisi inafanya kazi kuanzia asubuhi mpaka sakumi na mbili jioni

- **Masomo** yote yatafundishwa Kwa **lugha ya Kiingereza** isipokuwa Kiswahili kama somo, kuanzia darasa la awali hadi la saba, na lugha kuu ya mawasiliano akiwepo hapa shuleni ni kiingereza. Atafanya mitihani iliyoandaliwa na shule, Wilaya na Baraza la mtihani kama ilivyoelekezwa na Wizara ya Elimu. Masomo atakayofundishwa shuleni ni Hisabati, Sayansi, Jiografia, Historia, Tehama, Kiswahili, Uraia, Haiba na Michezo, na Kiingereza. Pia kutakuwa na somo maalumu la elimu ya kujitegemea (Home economy/ General knowledge).

**_BRIGHT STAR PRE AND PRIMARY SCHOOL_**
_P.O BOX 360 MAKAMBAKO, NJOMBE_
_CELL 0766617497/0714702045_
_Email. brightstarschooltanzania@gmail.com_
_Website. www.brightstarsschools.co.tz_

## ❖ FOMU YA USAJILI.

### A. MAELEZO YA MTOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Jina la kwanza** | | **Kati** | | **Mwisho** | |
| **Mahali alipozaliwa** | | | | **Tarehe ya kuzaliwa** | |
| **Umri.** | | **Dini** | | **Unapoishi kwa sasa** | |
| **Umbali kutoka nyumbani hadi shuleni (Km)** | | | | **Umeshasoma shule yoyote?** | |
| Shule aliyowahi kusoma (Kama jibu ni NDIO) | | | | | |
| Matatizo ya kiafya (kama yapo) | | | | | |
| Mambo anayopendelea (kama yapo) | | | | | |

### B. MAELEZO YA MZAZI/MLEZI

**i. BABA/ MLEZI**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Majina Matatu** | | | | | | |
| **Uhusiano** | | **Kazi** | | | | |
| **Simu ya mkononi** | | **Mtaa** | | | | |
| **Saini** | | | | | | |
| | | | | | | |

**ii. MAMA/ MLEZI**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Majina Matatu** | | | | | | |
| **Uhusiano** | | **Kazi** | | | | |
| **Simu ya mkononi** | | **Mtaa** | | | | |
| **Saini** | | | | | | |
| | | | | | | |

NB: Hakikisha unaambatanisha nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto wako.

BRIG HT STAR PRE

## B. SHERIA ZA SHULE

1. Mtoto asiyekuwa na sare hataruhusiwa kuingia shuleni. Watoto wa kike wa dini ya kiislam wataruhusiwa kuvaa hijabu ya rangi nyeupe.
2. Muda wa kuanza kufika shuleni ni saa 1:00 mpaka saa 2:00 asubuhi tu.
3. Ruhusa itatolewa shuleni pekee kwa maandishi.
4. Mtoto asiyelipia gharama ya usafiri hatachukuliwa na usafiri wa shule.
5. Mtoto asubirie usafiri na sio gari limsubiri mtoto.
6. Mafaili yanayoonesha maendeleo ya mtoto yatakuwa yanarudi mara mbili kwa mwaka (mwezi wa 6 na 12). Ukitaka kupata maendeleo ya mwanao uje uone shuleni.
7. Simu itapokelewa kuanzia saa 1:00 asubuhi – 12:00 jioni labda kukiwa na dharula.
8. **Wazazi tunapaswa kuandika majina ya mtoto kwenye sare zote za shule.**
9. Hereni, bangili wala cheni hazitakiwi shuleni, Nywele ziwe za uzi msuko wa masikio mawili/ Twende kilioni au Kilimanjaro. Pia zisiwekwe mapambo kichwani.
10. Mtoto asiyekuwa msafi hatachukuliwa kabisa
11. Mtoto asiyekuwa na mahudhurio mazuri kuanzia mwezi mmoja atafundishwa kwa makubaliano maalumu kati ya mwalimu na mzazi kwa gharama maalumu itakayolipwa na mzazi wa mtoto husika.
12. Vifaa vya mtoto vinavyohitajika shuleni vitakaguliwa siku ya kwanza mtoto atakaporipoti shule.
13. Mzazi asiyehudhuria vikao itabidi asikilize na kukubaliana na mawazo ya wazazi wengine waliyotoa wakati wa kikao.
14. Mtoto ataadhibiwa kutokana na sababu maalumu na kulingana na umri wake, pia nibaada ya mtoto mwenyewe kulitambua kosa lake.
15. Dawa kwa wanafunzi wagonjwa zikabidhiwe kwa mwalimu aliyetembea na gari pia kwa maelezo yaliyokamilika kuhusu matumizi ya dawa hizo. Pia mzazi unapaswa kukumbusha muda wa kutumia dawa hizo kwa njia ya simu.
16. **Viatu vya shule kwa wavulana ni rangi nyeusi, soksi nyeupe na raba nyeusi. Viatu vya shule kwa wasichana ni rangi nyeusi (Juma na Roza/ school fees), soksi nyeupe, raba nyeusi na Suruali ya rangi ya sketi. Pia Pull neck nyeusi kwa wote.**
17. Birthday parties (Sherehe za kumbukizi ya kuzaliwa mtoto) haziruhusiwi kufanyiwashuleni.

BRIGHT STAR PPE & PRIMARY SCHOOL

18. Kwa mzazi atayeshindwa kumpokea mtoto pindi magari yakipita kuwarudisha watoto majumbani atalazimika kutoa gharama ya Tshs. 5000/= kwa kila saa baada ya muda wa shule kuisha kwa ajili ya uangalizi wa mtoto.
19. Wahusika wa mtoto wanapaswa kujulikana. Hasa kwa wazazi wasioishi pamoja mfano waliotalakiana. Orodhesha watu wanaoruhusiwa kuja kumchukua au kumpokea mtoto.
20. Kutokufanya kazi ya nyumbani (home work) kwa kujirudia kutachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mtoto. Hivyo tunaomba umsimamie mwanao kazi za nyumbani anazopewa na walimu kila siku.
21. Inapotokea mzazi/mlezi hapatikani na mtoto ana tatizo la ugonjwa mzazi atatakiwakulipa gharama zote zilizotumika kwaajili ya matibabu ya mwanae.

**TAMKO LA MZAZI.**

- Nakubaliana na sheria zote za shule na nitatoa malipo yote ya ada kwa wakati.
  - Saini ya mzazi ______________________________
  - Tarehe ____________________________________

| | |
|---|---|
| | **BRIGHT STAR PRE AND PRIMARY SCHOOL**<br>P.O BOX 360 MAKAMBAKO, NJOMBE<br>CELL 0766617497/0714702045<br>*Email. brightstarschooltanzania@gmail.com*<br>*Website. www.brightstarsschools.co.tz* |

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**PART. A**
**TO THE MEDICAL OFFICER**
From: Designation_______ Division:_______________ Station________________
Please examine:
Mr. /Mrs. Miss___________________________________as to his/her fitness for appointment/ admission as a pupil in this school
Signature and official stamp_____

Date__

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by the medical officer)
I have examined the above and consider that he/she is physically fit/not fit for appointment as a pupil.
COMMENTS: ______

Name____________________________Signature________________Date_____________
Station_____ Designation ______

**NOTE:** Cancel inappropriate explanation/description.